**MUHIMU>Kuhakikisha kunakuwa na mipango ya matumizi sahihi ya bahari**

# Rais Samia: Uchumi wa buluu ni fursa

**Sasa agizo langu ni kwamba wizara zinazohusika na wadau wengine wote mjipange vizuri kulitumia Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika kupata masoko mazuri ya mazao yetu ya kilimo, mifugo na uvuvi kuboresha maisha ya watu wetu...**

**Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.**

NA MWANDISHI WETU, Zanzibar

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan amesema uchumi wa buluu ni fursa huku akiwataka wananchi kujipanga na kuweka mazingira mwafaka ya uwekezaji kunufaika kupitia rasilimali zinazopatikana katika sekta hiyo.

Dk. Samia alisema hayo katika sherehe za Msimu wa Pili wa Tamasha la Vyakula vya Baharini (Zanzibar Sea Food Festival) zilizofanyika ufukwe wa Kendwa, Mkoa wa Kaskazini Unguja, Zanzibar juzi.

Akisoma hotuba kwa niaba ya Rais, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega alisema maana halisi ya uchumi wa buluu ni matumizi endelevu ya rasilimali zilizomo katika bahari, maziwa na mito kwa maendeleo ya uchumi wa taifa.

Pia, kutengeneza ajira, kuleta ustawi wa maisha ya watu na kutunza afya ya maumbile ya bahari.

Alisema kupitia tamasha hilo vema kuzitumia fursa zilizopo na zinazojitokeza katika sekta ya uchumi wa buluu.

Alisisitiza fursa hizo ziwe endelevu ni muhimu kuhakikisha kunakuwa na mipango ya matumizi sahihi ya bahari, usimamizi bora wa ikolojia za bahari, kudhibiti uchafuzi wa bahari, kuimarisha uvuvi wa bahari kuu, kusimamia mnyororo wa thamani wa mazao ya baharini na kuimarisha mifumo ya kitaasisi ya usimamizi bora wa uchumi wa buluu na rasilimali zake.

Aliendelea kusema ni muhimu kuweka kipaumbele katika hifadhi ya mazingira ya bahari kwa kuwa bila kufanya hivyo hakutakuwa na upatikanaji endelevu wa samaki na mazao mengine ya bahari.

"Hili siyo suala la kitaifa tu, bali la kikanda na kimataifa. kama mnavyofahamu pamoja na kwamba mabadiliko ya tabianchi yanaathiri maeneo yote ya nchi, maeneo ya visiwa yapo hatarini zaidi. Hivyo, hatuna budi kulisimamia vyema suala la uhifadhi wa mazingira," alifafanua

Aidha, alibainisha mipango ya maendeleo ya kitaifa imeagiza kutekeleza ajenda ya uchumi wa buluu ya Tanzania, kama ilivyoainishwa katika Mpango wa 2050 kwa Zanzibar na Dira ya Maendeleo ya 2025 kwa Tanzania.

"Pamoja na maelekezo hayo, Ilani ya uchaguzi ya CCM 2020-2025 inatuelekeza kuongeza uzalishaji wa samaki na mazao ya baharini, ujenzi wa miundombinu ya uchumi, wa masoko ya kisasa na viwanda vya usindikaji wa samaki na ununuzi wa meli za uvuvi," alieleza.

Alisema kutokana na fursa zilizopo katika uchumi wa buluu ambazo zinaweka uhakika wa chakula nchini ni vyema Watanzania wakajipanga kupitia jukwaa la mifumo ya chakula Afrika linalotarajiwa kufanyika Dar es Salaam kuanzia Septemba 5 hadi 8, mwaka huu, nchi ililishe bara la Afrika kwa mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi.

"Sasa agizo langu ni kwamba wizara zinazohusika na wadau wengine wote mjipange vizuri kulitumia Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika kupata masoko mazuri ya mazao yetu ya kilimo, mifugo na uvuvi kuboresha maisha ya watu wetu," alisisitiza

**NMB KUIMARISHA UHUSIANO**

Wakati huo huo, Benki ya NMB ilitangaza kuendeleza dhamira yake ya kusaidia ukuaji wa sekta ya utalii na ajenda ya uchumi wa buluu ikiwa utekelezaji wa mkakati wake wa muda mrefu unaolenga kuunga mkono jitihada za kuongeza mchango wa sekta hizo, katika maendeleo ya kiuchumi Zanzibar.

Akizungumza na Rais Dk. Samia wakati wa maonyesho ya tamasha hilo, Mkuu wa Idara ya Biashara za Serikali wa NMB Vicky Bishubo, alisema kwa miaka mingi sasa, benki hiyo imekuwa ikishirikiana kwa karibu na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuimarisha ukuaji wa sekta ya utalii na ajenda ya uchumi wa buluu kuchangia ukuaji wa Pato la Taifa la Zanzibar (GDP).

"Sisi benki ya NMB, tumeanzisha suluhisho mbalimbali la kibenki kuchangia juhudi za serikali kuinua mchango ya sekta za utalii na ajenda ya uchumi wa buluu ikiwa utekelezaji wa azma yetu ya kuhakikisha sekta hizo zinachangia zaidi uchumi wa Zanzibar kwa ujumla," alisema.

Vicky alibainisha benki hiyo tayari imetia saini mkataba wa makubaliano na Shirika la bandari Zanzibar (ZPC) kuanzisha mfumo jumuishi ambao pamoja na mambo mengine utawawezesha wafanyabiashara kulipa kodi kwa kutumia mfumo wa udhibiti namba yaani (control number).

"Mfumo huu pamoja mambo mengine unalenga kurahisisha mchakato wa malipo na kwa kiasi kikubwa utaokoa muda kwa wafanyabiashara na kuhakikisha uwazi kwa serikali katika ukusanyaji wa mapato," alisema.

Aliongeza benki hiyo pia imeshirikiana na Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) kuunda mfumo wa pamoja unaolenga kurahisisha mchakato wa uwekezaji visiwani humo.

**MAONYESHO**




RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan, akipata maelezo kutoka kwa Mkuu wa Idara ya Biashara za Serikali wa Benki ya NMB, Vicky Bishubo, alipotembelea banda la benki hiyo, wakati wa Maonyesho ya Chakula cha Baharini 2023 yaliyofanyika katika Ufukwe wa Kendwa, Mkoa wa Kaskazini Unguja, Zanzibar, mwishoni mwa wiki. Kulia ni Mkuu wa Idara ya Masoko wa benki hiyo, Rahma Mwapachu na wa pili kulia ni Mkuu wa Idara ya Mtandao wa Matawi ya benki ya NMB, Donatus Richard. (Na Mpiga Picha Wetu).

CamScanner